

MIKUTANO YA KUPATA MAONI KUHUSU MAOMBI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA YA DAR ES SALAAM (DAWASA).

Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imepokea ombi Na. **TR-W-09-001** kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Dar es Salaam (DAWASA) ya kurekebisha bei ya huduma inazotoa.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, EWURA inanzisha taftishi ya kupata maoni ya wadau ili kujua uhalali wa maombi iliyopokea. Hivyo, EWURA imeandaa mikutano itakayofanyika katika maeneo husika kama ilivyoelekezwa hapo chini.

Mikutano hiyo itawashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo Baraza la Wawakilishi wa Watumiaji wa huduma (EWURA-CCC); Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) pamoja na wananchi kwa ujumla.

Mikutano Taftishi ya Wazi

Na.	Mamlaka	Mwisho wa kusajili watoa maoni	Tarehe ya Taftishi	Muda	Mahali
1.	DAWASA/DAWASCO	21 MEI,2009	27,MEI 2009	SAA 4 ASUBUHI	UKUMBI WA KARIMJEE-DAR
2.	DAWASA/DAWASCO.	21 MEI, 2009	28, MEI,2009	SAA 4 ASUBUHI	UKUMBI WA NJUWENI-KIBAHA

Wadau wanaopenda kutoa maoni yao kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi cha wiki mbili baada ya mikutano hiyo.

Wadau pia watakaopenda kuweka pingamizi wanatakiwa kuonesha nia yao kwa kuiandikia EWURA. Wadau wote watakaoweka pingamizi watapata muda kuwasilisha maoni yao katika mikutano hiyo na pia watakuwa na fursa ya kupata nyaraka zote zilizowasilishwa na waombaji kwa kulipia gharama kidogo za kudurufu nyaraka hizo.

Nakala za maombi na nyaraka za Mamlaka hizo zilizowasilishwa EWURA zinaweza kusomwa na mtu yeyote wakati wa saa za kazi kati ya saa 3 asubuhi na saa 11 jioni katika ofisi za EWURA kwa anuani iliyotajwa hapo juu.

Wadau wanaombwa kuzingatia muda uliopangwa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo juu ili kufanikisha zoezi hilo.

**Ufafanuzi zaidi unaweza kupatikana kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu wa
EWURA.**